



MTIHANI WA BIBLIA (part 14) (MASWALI YA BIBLIA)

1. Kwanini Mfalme Daudi hakumjengea Mungu hekalu?

2. Sulemani alikuwa na wake wangapi?

3. Jemedari wa jeshi la Sauli alitwa nani?

4. Kuhani wa kwanza kwenye biblia alikuwa ni nani?

5. Mtoto wa Yezebeli alitwa nani

6. Je ni watu gani waliokuwa wapinzani wa Nehemia katika kuujenga Yerusalemu?

7. Katika biblia ni nani ambaye punda wake aliongea na kwanini?

8. Hadasa ni nani katika biblia?

9. (Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani) je kifungu hiki kinapatikana wapi katika biblia

10. Kitabu cha ufunuo Yohana, Mtume Yohana alikiandika akiwa wapi?

Nakutakia mtihani mwema Mjoli wa Bwana.



@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618

02/03/2023

MASAHIHISHO YA MTIHANI LEO

MTIHANI WA BIBLIA (part 14)
(MASWALI YA BIBLIA)

1.Kwanini Mfalme Daudi hakumjengea Mungu hekalu?

Jibu. 1)Kwasababu Daudi mikono yake ilimwaga damu nyingi sana

Soma. 1Nyakati 22:7-8

2)Alikuwa amezungukwa na maadui wengi

Soma 1wafalme 5:3

2.Sulemani alikuwa na wake wangapi?

Jibu. 1000

Ambapo wake 700 na masulia 300

Soma 1Wafalme 11:1-3

3. Jemedari wa jeshi la Sauli alitwa nani?



Jibu. ABNELI

Soma. 1Samweli 14:50

4.Kuhani wa kwanza kwenye biblia alikuwa ni nani?

Jibu. MELKIZEDEKI

Soma. Mwanzo 14:18

5.Mtoto wa Yezebeli aliitwa nani?

Jibu. ==Athalia 2Wafalme 8;18

==Yoramu 2wafalme 8-16

6.Je ni watu gani waliokuwa wapinzani wa Nehemia katika kuujenga Yerusalemu?

Jibu. SANBALATI NA TOBIA NA GESHEMU (Wengine walikuwa nyuma ya hawa)

Soma .Nehemia 4:2

7.katika biblia ni nani ambaye punda wake aliongea na kwanini?

Jibu. BAALAMU

Sababu. Aliongea kwasababu alipigwa na Baalam nabii wa uongo alipokuwa akitaka kwenda kuwa laani Israeli kwa mfalme Balaki

Ukihitaji habari zaidi kijifunza zaidi juu ya Baalam nabii wa uongo nitafute kwa namba hizi
0652274252 au 0693036618

8.Hadasa ni nani katika biblia?

Jibu. Malkia ESTA

Soma. Esta 2:7



9. (Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani) je kifungu hiki kinapatikana wapi katika biblia

Jibu. 1petro 1:5

10. Kitabu cha ufunuo Yohana ,Mtume Yohana alikiandika akiwa wapi?

Jibu. Katika kisiwa cha PATMO

Soma. Ufunuo 1:9

BWANA YESU akubariki sana Mjoli wa Bwana.

@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618